**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**KANDA YA TABORA**

**MAOMBI YA MADAI NA. 2 YA 2022**

**THOMAS HERMAN LILANDIMA ................................ MWOMBAJI WA 1**

**IRENE HERMAN LILANDIMA .....................................MWOMBAJI WA 2**

**REDEMTA HERMAN LILANDIMA ...............................MWOMBAJI WA 3**

**SAMWEL HERMAN LILANDIMA ................................MWOMBAJI WA 4**

**ELIZA HERMAN LILANDIMA ..................................... MWOMBAJI WA 5**

**CECILIA HERMAN LILANDIMA ...................................MWOMBAJI WA 6**

**DHIDI YA**

**GENEROZA NGAYEKAMWE BUKURA ...............MJIBU MAOMBI WA 1**

**ABEL HERMAN LILANDIMA ...............................MJIBU MAOMBI WA 2**

**SKOLASTIKA HERMAN LILANDIMA ...................MJIBU MAOMBI WA 3**

**ATHANAS HERMAN LILANDIMA .........................MJIBU MAOMBI YA 4**

**UAMUZI**

*Tarehe : 4/4/2022 & 8/4/2022*

**BAHATI SALEMA,J.:**

Uamuzi huu unatokana na maombi yaliyofunguliwa mahakamani hapa baada mvutano uliojitokeza kati ya ndugu kumi wanaovutana kuhusu mahali pa kumzika ndugu yao Marehemu **Herman Lilandima** aliyefariki tarehe 31/03/2022 katika Hospitali ya rufaa Kitete mkoani Tabora.

Maombi haya yaliletwa mahakamani hapa kwa hati ya dharura chini ya kifungu namba 68(e) na 95 cha Sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 33 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019 na kifungu namba 2(3) cha Sheria ya Kuongoza Matumizi ya Sheria (JALA) Sura ya 358 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Waombaji wote sita kwa pamoja wanaiomba mahakama itoe amri zifuatazo: -

1. Kwamba, Mahakama itoe amri ya kuwa mwili wa marehemu **HERMAN LILANDIMA @ HELMAN LILANDIMA** uzikwe huko Kahama.

2. Kwamba, mwili wa marehemu uwekwe chini ya uangalizi wa waombaji kwa ajili ya taratibu za maziko huku wakisubiri ufunguaji wa shauri la usimamizi wa mirathi.

3. Zuio la kudumu litolewe dhidi ya wajibu maombi, mawakala wao au wawakilishi wao kutokuutoa mwili wa marehemu katika chumba cha kuhifadhia maiti kwa ajili ya maziko au kuingilia taratibu za mazishi zinazoandaliwa na waombaji.

4. Amri yoyote ambayo mahakama itaona inafaa kutolewa.

Maombi haya yaliambatanishwa viapo vya waombaji ambavyo viliambatana na nakala ya walichokiita kuwa ni wosia wa marehemu Helman Lilandima pamoja na nakala ya barua ikiwa inaonesha kuwa

iliandikwa na marehemu kabla ya kifo chake akielekeza ni wapi atazikwa pindi atakapokufa.

Historia kama inavyopatikana kwenye rekodi za shauri hili ni kwamba, Marehemu Herman Lilandima wakati wa uhai wake aliwahi kumuoa mjibu maombi namba moja Generoza Ngayekamwe Bukura wakafanikiwa kupata watoto na baadae kutengana. Pia marehemu aliwahi kuwa na mahusiano na wanawake wengine tofauti na mjibu maombi namba moja na kufanikiwa kupata nao watoto na kufanya watoto wake kuwa kumi na nane.

Shauri hili lilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa waombaji wote waliwakilishwa na wakili msomi Kelvin Kayaga huku wajibu maombi wakiwakilishwa na wakili msomi Charles Ayo.

Katika mawasilisho yake wakili Kayaga aliieleza Mahakama kuwa Herman Lilandima sasa ni marehemu alifariki tarehe 31/03/2022 katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete, aliongeza kuwa pande zote mbili katika shauri hili zinakinzana juu ya wapi mwili wa marehemu utakapozikwa. Wakili Kayaga aliendelea kueleza kuwa matakwa ya marehemu yalikuwa ni kuzikwa huko Kahama mkoani Shinyanga pindi atakapoaga dunia.

Akisisitiza kuhusu jambo hilo, wakili Kayaga alieleza kuwa wakati wa uhai wake marehemu alitamka mara nyingi juu ya nia yake ya kuzikwa huko Kahama-Shinyanga. Pia tarehe 23/03/2022 marehemu

alipokuwa katika Kituo cha Afya Omulinga aliwasisitizia mwombaji namba 2 na namba 3 juu ya nia yake ya kuzikwa huko Kahama na akataka mwombaji namba 1 afike.

Wakili Kayaga aliongeza kuwa, tarehe 06/04/2007 marehemu aliandika wosia pamoja na barua ya maelekezo ya mahali atakapozikwa na kuvipeleka Mahakama ya Mwanzo Isevya tarehe 09/07/2007, katika wosia huo alimtaja mwombaji namba moja asimamie matakwa yake hayo. Wakili alieleza kuwa wajibu maombi wanapinga maelezo hayo ndiyo sababu imewafanya kufika mahakamani hapa.

Zaidi, wakili Kayaga aliongeza kuwa upande ya waleta maombi hawana maslahi yoyote yale na mali za marehemu isipokuwa ni wajibu wao kisheria kufuata matakwa ya marehemu hivyo hoja pekee inayojitokeza ni endapo matakwa ya marehemu yana uzito wowote pale inapotokea ameacha namna ambavyo anataka mwili wake uhifadhiwe.

Kwa kumalizia wakili Kayaga alieleza kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Sura ya 2 pamoja na mambo mengine inaongelea haki ya kuishi pamoja na mtu kuwa na haki ya kuchagua mtindo wa maisha na kutokana na haki hiyo anaamini kwamba mtu anaweza kuchagua mwili wake uzikwe wapi na kwa kufanya hivyo hakuna sheria ambayo imekiukwa.

Katika kujibu hoja hizo, Wakili Charles Ayo alipinga maombi ya kuwa mwili wa marehemu uzikwe Kahama, maombi ya mwili wa marehemu kuwa chini ya uangalizi wa waombaji na pia alipinga ombi la amri ya zuio la kudumu kuzuia wajibu maombi kuuondoa mwili wa marehemu kutoka kwenye chumba cha kuhifadhia maiti.

Wakili Ayo aliendelea kueleza kuwa ni maombi ya wajibu maombi kwamba mwili wa marehemu uzikwe huko Kigoma alipozaliwa na kama itashindikana basi uzikwe Tabora mahali ambapo alikuwa anaishi ili pande zote mbili ziwe katika nafasi nzuri ya kuzuru kaburi la marehemu.

Kuhusu hoja iliyowasilishwa na waombaji kwamba mjibu maombi namba 1 alitengana na marehemu, hoja hiyo ilipingwa vikali na upande wa wajibu maombi kwa kusema kuwa hakuna ushahidi wowote uliotolewa kuthibitisha jambo hilo.

Pia, katika hoja ya kuwa, kwa nyakati tofauti marehemu alitoa taarifa kwa mwombaji wa kwanza kwamba mwombaji achukue jukumu la kuhakikisha mwili unazikwa Kahama, upande wa wajibu maombi walipinga hoja hiyo kwa sababu hakuna uthibitisho wowote ulioletwa kuweza kuthibitisha hilo. Na kama kweli alitamka matakwa yake hayo kwa binti zake Irene na Redempta basi alifanya hivyo akiwa katika hali ya ugonjwa.

Kuhusu nakala ya wosia iliyoambatanishwa katika kiapo cha mjibu maombi namba 1 kama Kiambatanisho APP1, wakili Ayo alieleza kuwa kiambatanisho hicho kinakosa sifa ya kuitwa Wosia kwa sababu hakikuwa na mashahidi wanaotakiwa kisheria kushuhudia wakati wosia unaandikwa na pia wosia huo umewataja baadhi ya Watoto na kuwaacha wengine kitu ambacho kinaufanya wosia huo kukosa vigezo.

Pia, kuhusu hoja iliyoibuliwa na wakili wa waombaji kwamba waombaji hawana maslahi yoyote katka mali za marehemu wakili Ayo ameeleza kuwa hoja hiyo haina ukweli wowote na pia aliongeza kuwa hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kwamba mjibu maombi namba 1 alipewa talaka na kwamba mjibu maombi namba 2, 3 na 4 wote ni watoto wa marehemu. Wakili Ayo aliiomba mahakama iyakatae maombi ya waombaji na kuwaruhusu wajibu maombi washiriki katika shughuli zote za kuusitiri mwili wa marehemu huku Kigoma anakoishi mama yake mzazi au azikwe Tabora ambapo pande zote zitakuwa na nafasi ya kuzuru kaburi la marehemu.

Katika kujibu hoja za wakili wa wajibu maombi, wakili wa waombaji aliiomba mahakama kutokuzingatia maelezo ya upande wa utetezi kwani hayakuletwa kwa kiapo, Wakili Kayaga aliendelea kueleza kuwa kwa kuwa upande wa wajibu maombi wameshindwa kuleta kiapo kinzani (counter-affidavit) ni wazi kwamba wameshindwa kupinga maombi ya waombaji.

Kuhusu nakala ya wosia wakili Kayaga wa upande wa waombaji alikubali kuwa haina vigezo vya kuitwa wosia lakini inaelezea wazi matakwa ya marehemu. Aliongeza kuwa kilicholetwa mahakamani hapa siyo suala la uhalali wa wosia isipokuwa ni kutimiza matakwa ya marehemu alivyohitaji kuzikwa huko Kahama.

Wakili Kayaga alisisitiza kuwa hakuna sababu za msingi za kukataliwa kwa maombi haya na waombaji hawakatai ushiriki wa wajibu maombi kwenye mazishi na kwa kutii matakwa ya marehemu si ubaguzi kwa hiyo hata kama mahakama itatoa amri kwamba matakwa ya marehemu yaheshimiwe hata wajibu maombi hawatakatazwa kushiriki kumzika marehemu.Hivyo aliiomba mahakama kukubali maombi yao.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili Mahakama hii imeyapitia maelezo yote yaliyotolewa na baada ya kuyazingatia imeona mambo mawili ya msingi ambayo mahakama hii inatakiwa iyatolee amri.

i. *Ni nani mwenye haki ya kuuzika mwili wa marehemu Herman Lilandima*
ii. *Ni wapi mwili wa marehemu Herman Lilandima unatakiwa kuzikwa*

Kabla sijatolea maamuzi mambo hayo hapo juu nimeona ni vyema kufafanua hoja moja iliyohusu upande wa wajibu maombi kutokuwasilisha kiapo kinzani kama ilivyoibuliwa na wakili wa waombaji Kelvin Kayaga.

Kama ilivyowahi kuamuliwa katika kesi nyingi katika mahakama hii, kutokuwasilisha kiapo kinzani haimaanishi kwamba maombi hayajapingwa na upande wa wajibu maombi, kawaida ni kwamba wajibu maombi wanayo nafasi ya kufika mahakamani wakati wa kusikilizwa na kupinga maombi hayo kwa mdomo. Mahakama ya rufani katika kesi ya ***The Editor Msanii Africa Newspaper vs Zacharia Kabengwa, Civil Application No. 2 of 2019*** iliamuliwa kwamba: -

> *"Kama mjibu maombi akiamua kutokuleta kiapo kinzani,haitamaanisha kwamba maombi hayajapingwa. Licha ya kuwepo kiapo kinzani bado mjibu maombi anaweza kufika mahakamani na kupinga maombi."*

Katika maombi haya, ni kweli wajibu maombi hawakuwasilisha kiapo kinzani lakini walifika mahakamani wakiwakilishwa na wakili msomi Charles Ayo kupinga maombi haya hivyo kwa msingi wa maamuzi katika kesi tajwa hapo juu, mahakama hii imeshindwa kukubaliana na hoja ya wakili wa waombaji kwamba maombi haya hayakupingwa. Hata hivyo wajibu maombi wameshindwa kuisaidia mahakama ipasavyo kwa kushindwa kujibu kiapo cha waombaji.

Nikirejea katika hoja ya kwanza kuwa ni *nani mwenye haki ya kuuzika mwili wa marehemu Herman Lilandima*. Katika sheria za Tanzania hakuna sheria inayoeleza kuwa ni mtu gani anatakiwa apewe haki ya kumzika mwingine isipokuwa katika mazingira yetu mara

nyingi haki ya kuzika ipo kwa wanafamilia ya marehemu au mwenza wa marehemu.

Katika shauri hili japo zilijitokeza hoja za kwamba mjibu maombi namba moja Generoza Ngayekamwe Bukura ambaye ni mke wa marehemu aliwahi kutengana na mumewe mwaka 1990 hoja hii haikuweza kuthibitishwa kwa namna yoyote kwamba aliwahi kutengana na mumewe hivyo inabaki kwamba mjibu maombi ni mke wa marehemu na wengine wote wanaosalia katika shauri hili ni watoto wa marehemu Herman Lilandima.

Kimsingi hakuna mtu mwenye haki ya kuumiliki mwili wa mtu mwingine pale anapofariki kwani mwili wa mtu siyo mali inayofaa kumilikiwa, kama nilivyoeleza hapo juu wanafamilia au ndugu wa karibu wa marehemu ndiyo wanaokuwa na wajibu wa kuuzika kwa heshima mwili wa ndugu yao anapokufa.

Katika shauri hili waombaji wote na wajibu maombi wote ni ndugu wa karibu wa marehemu kwa maana ya kwamba ni mama,mke na watoto wa marehemu, wote hao wanao wajibu wa kuuzika mwili wa ndugu yao bila kubaguliwa. Kwa sababu hiyo ombi la pili la kuweka mwili wa marehemu katika uangalizi wa waombaji na lile la tatu la kutoa zuio la kudumu kwa wajibu maombi linakataliwa na mahakama hii.

Nikirejea katika hoja ya pili kwamba *ni wapi mwili wa marehemu Herman Lilandima unatakiwa kuzikwa*, kwanza upande wa waombaji unaomba mwili wa marehemu uweze kuzikwa huko Kahama ili kutimiza maelekezo aliyoyatoa marehemu na upande wa mjibu maombi unapinga maelekezo hayo na kuomba mwili wa marehemu uzikwe Kigoma alikozaliwa marehemu na anapoishi mama yake mzazi au uzikwe Tabora alipokuwa akiishi marehemu.

Katika kutetea jambo hili upande wa waombaji ulieleza kwamba marehemu wakati wa uhai wake mara kadhaa alimtamkia mwombaji namba 1 kuwa endapo atafariki mwombaji huyo ahakikishe mwili wake unazikwa huko Kahama mkoani Shinyanga. Pia mwombaji huyo alipewa taarifa juu ya uwepo wa barua zilizoachwa na marehemu na kuelekeza kwamba mwombaji namba 1 apatiwe pale atakapofariki na alipofariki alikabidhiwa barua hiyo na alipoifungua akakuta ni wosia wa marehemu.

Ni dhahiri kwamba katika jamii za watanzania suala la mazishi hutofautiana katika mila, desturi, tamaduni na taratibu kutokana na jamii husika anayotoka marehemu. Hivyo mahakama hii ilitegemea ifahamishwe ipasavyo kuhusu jamii aliyotokea marehemu, kabila lake, dini yake na hata mtindo wake wa maisha ukizingatia kwamba marehemu alikuwa mtu mzima. Jambo ambalo halikuelezwa na pande zote mbili.

Jambo pekee ambalo mahakama hii iliarifiwa na upande wa waombaji ili iweze kutoa maamuzi ni kwamba marehemu alimuoa mjibu maombi namba moja na pia aliwahi kuwa na mahusiano na wanawake wengine. Kwa upande wa wajibu maombi japo ilipingwa na waombaji waliongeza kwamba asili ya marehemu ni Kigoma na mama yake mzazi bado yupo hai na pia marehemu ameacha watoto kumi na nane.

Kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa na upande wa waombaji, hakuna popote ilipoelezwa kama marehemu ana asili ya Kahama au ana mji huko Kahama, bali ushahidi wa Wosia na barua ya maelekezo ya mahali pa kuzikwa marehemu karibu na kaburi la marehemu mke wake Hadija unatia wasiwasi kwani ushahidi huo unaegemea zaidi upande mmoja wa waombaji kama vile marehemu hakuwahi kuwa na familia nyingine zaidi ya waombaji peke yao.

Nikigusia kidogo kuhusu wosia ambao unasemekana uliwasilishwa katika mahakama ya mwanzo Isevya-Tabora mwaka 2007, mahakama hii inaona kuwa wosia huo unatia mashaka kwani hakuna shahidi yeyote aliyemshuhudia marehemu akiuandika, vilevile katika barua iliyoelekeza mahali atakapozikwa marehemu, hakuna shahidi yeyote aliyemshuhudia marehemu akiandika barua hiyo, jambo hili linatia mashaka kwani hata uhifadhi wa wosia huo na barua ni wa mashaka.

Kwa mantiki hiyo itoshe kusema kuna walakini mwingi kwenye uhalali wake hata wakili wa waombaji, Kayaga alikiri hilo.

Hali kadhalika katika Mahakama ya Rufani, shauri la **Ramnik Vaghellah dhidi ya Mahendra Vaghellar,**[2000] TLR 223 ilieleza kuwa ili wosia uweze kutekelezeka ni lazima uwe halali.Jambo ambalo kwa sasa mahakama hii haiwezi kulizungumzia.

Ushahidi uliotolewa unaonyesha kwamba marehemu aliwahi kuwa na mwanamke huko Kahama mkoani Shinyanga na mwanamke huyo sasa ni marehemu lakini hakuna uthibitisho kwamba marehemu amewahi kuwa na mji huko Kahama au kumiliki kiwanja ambacho anaweza kuzikwa huko Kahama-Shinyanga. Ukiangalia wosia uliodaiwa kuandikwa na marehemu unasema kwamba anamiliki nyumba moja ya vyumba sita iliyopo mtaa wa Isevya-Tabora, wosia huo haujataja chochote alichoacha marehemu huko Kahama. Pia maelezo ya waombaji kuwa marehemu alitamka mara kadhaa hayana ushahidi wowote kuthibitisha kama kweli marehemu aliyatamka hayo.

Upande wa wajibu maombi walieleza kuwa mama mzazi wa marehemu anaishi Kigoma na ameweza kufika mahakamani hapa akiambatana na mjibu maombi namba moja, suala ambalo halikupingwa hata kidogo na waombaji jambo ambalo limefanya mahakama hii iamini kwamba asili ya marehemu ni Kigoma na siyo Kahama.

Kwakuwa mahakama hii imeshindwa kuuamini ushahidi wa waombaji kuwa marehemu alitamka kwamba azikwe Kahama, hoja inayobaki ni je, marehemu anatakiwa kuzikwa wapi. Nadhani hoja hii haiihitaji kutupotezea muda cha msingi ni kuangalia maisha aliyokuwa anaishi marehemu wakati wa uhai wake.

Katika shauri la **Innocent Mbilinyi:** (Deceased),(1969) HCD Na. 283 mahakama iliangalia namna ya maisha aliyokuwa akiishi marehemu.

Ushahidi unaonyesha kwamba, marehemu alikuwa mkazi wa Tabora hadi umauti ulipomfika, japokuwa imeelezwa kuwa mama wa marehemu ni mkazi wa Kigoma hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba marehemu ana makazi huko Kigoma, hivyo sehemu pekee inayofahamika kuwa ni makazi rasmi ya marehemu ni Tabora na kwa sababu hiyo sehemu sahihi au muafaka ya kuuzika mwili wake ni Tabora ili pande zote mbili pamoja na ndugu, jamaa na wanafamilia wa marehemu waweze kushiriki kuuzika mwili wa marehemu Herman Lilandima na kuweza kuzuru pale inapobidi.

Baada ya kusema hayo, Mahakama hii imefikia uamuzi kwamba maombi ya waombaji hayana msingi wowote hivyo yanatupiliwa mbali na pia mahakama hii inatoa amri kuwa shughuli za mazishi zifanyike Tabora ambapo itatoa fursa kwa watu wote wenye nia ya kushiriki mazishi hayo kuliko kwingineko bila kubaguliwa.Gharama zinazohusiana na marehemu zilipwe na pande zote mbili.

Hii ndiyo amri ya Mahakama.

**A.BAHATI SALEMA**

**JAJI**

**8/4/2022**

Uamuzi huu umesomwa leo hii tarehe 8/4/2022 mbele ya waombaji na wajibu maombi.

**A. BAHATI SALEMA**

**JAJI**

**8/4/2022**

Haki ya rufaa imeelezwa.

**A. BAHATI SALEMA**

**JAJI**

**8/4/2022**

THE HIGH COURT OF TANZANIA